

MKATABA WA PANGO

**KATI YA**

ERNEST MWAIPUNGU

**NA**



*Erick Byansheko*

FJ DAYWELL SERVICES LIMITED

**UMETAYARISHWA:-**

ERICK BYANSHEKO,  
(ADVOCATE),  
P. O. BOX 71908,  
DAR ES SALAAM.

## MKATABA WA PANGO

MKATABA HUU WA UPANGISHAJI umesainiwa leo tarehe 20.....  
mwezi Machi.....2025.

### KATI YA

**ERNEST MWAIPUNGU** wa S.L.P ....., Dar es Salaam, (ambaye atatambulika kama "**MWENYE ENEO**" katika mkataba huu, tafsiri ambayo itatambuliwa pia kwa mtu yeyote mwenye uhusiano na "**MWENYE ENEO**" aidha awe ni mwakilishi au mrithi wake) kwa upande mmoja.

### NA

**FJ DAYWELL SERVICES LIMITED** wa S.L.P.....16660 Dar es Salaam, Simu 0716780070 (ambaye atatambulika kama "**MPANGAJI**" katika mkataba huu, tafsiri ambayo itatambuliwa pia kwa mtu yeyote mwenye uhusiano na mpangaji aidha awe ni mwakilishi binafsi au mrithi wake) kwa upande mwingine.

### INATHIBITISHWA kwamba:-

1. Mwenye eneo anapangisha kwa Mpangaji eneo lake lenye mita za eneo 3000 lililopo Buza Kanisani, wilaya ya Temeke, Dar es Salaam kwa shughuli za biashara ya baa kuanzia tarehe **20 mwezi Machi, 2025** kwa kipindi cha miaka mitatu (yaani miezi 36) na kwamba kodi ya pango italipwa kwa mkupuo wa miezi 12 (mwaka mmoja) na kodi ya pango itakuwa ni malipo ya **shilingi milioni moja na laki tatu (1,300,000/= TZS)** tu kwa kila mwezi.
2. Mkataba huu utakoma tarehe **20 mwezi Machi, 2028** huku malipo yakifanyika kwa mkupuo wa miezi kumi na miwili.
3. Kwahiyo malipo ya mwaka wa kwanza yatakuwa ni **15,600,000/= TZS (Milioni kumi na tano laki sita)** ambayo yatalipwa kupitia akaunti namba 0112268067400 CRDB, Jina ni **ERNEST MWAIPUNGU**
4. Mpangaji anaingia makubaliano na Mwenye eneo kama ifuatavyo:-
  - a) Amelipa kiasi cha **15,600,000/= (Shilingi Milioni kumi na tano laki sita)** tu baada ya kusainiwa kwa mkataba baina ya pande mbili husika ikiwa ni kodi ya miezi kumi na miwili (mwaka mmoja);
  - b) Kwamba, biashara ambayo itafanyanyika katika eneo husika ni kuegesha maloli (parking)



- c) Kwamba, mpangaji hatorithisha au kupangisha au kutoa eneo bila idhini ya Mwenye eneo;
  - f) Kwamba, eneo alilopangishwa litakuwa ni kwa shughuli za biashara tu;
  - g) Mwisho wa mkataba au panapo majadiliano ya kuendelea au kutoendelea na mkataba eneo liwe katika hali na mazingira mazuri;
5. Mwenye eneo anaingia makubaliano na Mpangaji kwamba:-
- a) Mwenye eneo au mtu yeyote mwenye haki juu ya eneo hilo anaahidi kutoingilia upangaji na maisha ya Mpangaji katika kipindi chote cha upangaji endapo atazingatia masharti na makubaliano yaliyomo katika mkataba huu.
  - b) Mwenye eneo ameruhusu Mpangaji aweke nyenzo zote za kazi/ biashara ya maegesho kwa kipindi chote cha upangaji.
  - c) Mpangaji atalipa tozo za aina zote zinazohusiana na biashara yake kwenye eneo husika isipokuwa kodi ya ardhi italipwa na Mwenye eneo.

5. **IZINGATIWE NA INAKUBALIWA KWAMBA:-**

- a) Ikiwa makubaliano yoyote ya upangaji kwa upande wa Mpangaji hayatafuatwa au kuzingatiwa, Mwenye eneo atakuwa na haki kisheria kuingia katika eneo hilo na mkataba huu wa upangaji utatumika kuamua hatima ya ukiukwaji huo wa makubaliano.
- b) Mwenye eneo hatahusishwa na lolote lile endapo ajali au madhara yeyote yatatokea kwa Mpangaji au mtu mwenye ruhusa ya mpangaji kuingia katika eneo lililopangwa, au kitu chochote, watumishi mwakilishi au mtu yeyote au mali yoyote katika eneo.
- c) Kwamba, kwa namna yoyote ile mkataba huu ni kwa ajili ya kudumu miaka mitatu endapo mkataba huu utazingatiwa.



- d) Mkataba wa upangaji unaweza kuendelezwa endapo mpangaji atatuma maombi kwa mwenye eneo kuhusu kuongeza muda wa upangaji miezi mitatu kabla ya kuisha kwa muda wa mkataba.
6. Taarifa yoyote chini ya mkataba huu itakuwa katika maandishi na taarifa yoyote kwa Mpangaji itachukuliwa kuwa imefika endapo imeandikwa kwa njia ya Posta, email, meseji ya simu au watsap ya Mpangaji, au barua kupelekwa kwenye makazi yake ya mara ya mwisho mahali popote pale alipokuwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taarifa yoyote kutoka kwa Mwenye eneo itachukuliwa kuwa imemfikia mpangaji au mtu yeyote mwenye idhini yake kuipokea au siku tatu tangu barua itumwe kwa njia ya posta.

**INATHIBITISHWA** na pande zote mbili kuwa mkataba huu umesainiwa katika tarehe na mwaka kama inavyoonekana.

**IMESAINIWA na KUTOLEWA** hapa Dar es Salaam na }

**ERNEST MWAIPUNGU** mbele yangu }

leo tarehe 20 mwezi Machi, 2025 }

E. Mwaipungu

Sahihi

Anuani

Sifa

[Signature]

S.L.P 7908

DAR ES SALAAM

WAKILI



**IMESAINIWA na KUTOLEWA** hapa Dar es Salaam na }

**FJ DAYWELL SERVICES LTD** kupitia **FURAHA** }

**LANGSON MWAKAGILE (MKURUGENZI MTENDAJI)** }

mbele yangu leo tarehe 20 mwezi Machi, 2025 }

[Signature]

Sahihi

Anuani

Sifa

[Signature]

S.L.P 7908

DAR ES SALAAM

WAKILI

